

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ مَأْمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لِيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَنْتُمْ تَخْلُفُونَ  
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَمْ يُمْكِنَ لَهُمْ دِينُهُمُ الْأَقْرَبُ لَهُمْ وَلَكُبُرُّهُمْ مِنْ بَعْدِ حَوْفِهِمْ أَنَّهُمْ  
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ



Jumanne, 1 Jumada II 1446 H

03/11/2024 M

Na: 1446 / 08

### Tanzia ya Mbebaji Ulinganizi

[مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رَجُلٌ صَدَقَوَا مَا عَاهَدُوا اللَّهُ عَلَيْهِ فَيُنْهِمُ مَنْ قَضَى نَحْبَهُ وَمَنْهُمْ مَنْ يَنْتَظِرُ وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلًا]

“Mionganini mwa Waumini wapo watu walio timiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo.” [Al-Ahzab:23]

(Imetafsiriwa)

Kwa imani katika qadhaa ya Mwenyezi Mungu (swt) na kutaka malipo Yake, Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir / Wilayah Jordan inamuomboleza Mbebaji Da'wah katika safu zake:

**Hajj Mustafa Abdullah Al-Issa Al-Jaber Al-Aboushi (Abu Anas)**

Aliyefariki kwenda kwenye rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu asubuhi ya leo, Jumanne, 3/12/2024, akiwa na umri wa miaka 80.

Abu Anas alitumia miaka yake kubeba Dawah kwa ajili ya kurudisha mfumo kamili wa maisha wa Kiislamu kuititia kusimamisha Khilafah Rashida. Alijiunga na Hizb ut Tahrir mapema katika ujana wake na alikuwa mvumilivu, mkakamavu, na mwenye bidii katika kutangaza haki. Alifungwa katika safari yake ya da'wah katika jela za madhalimu na akabaki imara katika kubeba Dawah hadi kifo chake, alikuwa mkweli kwa yale aliyomuahidi Mwenyezi Mungu. Sisi tunamhisabu kuwa hivyo na wala hatumtakasi ye yote kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ndiye mhasibu wake.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu amrehemu kwa rehema yake inayokizunguka kila kitu, amuingize katika Jannah yake pana, na amjaalie kuwa mionganini mwa watu wa Al-Firdaus Al-A'la (Pepo ya juu kabisa) pamoja na Mitume, wakweli, mashahidi, na watu wema - na hao ni maswahaba bora walioje. Vile vile tunamuomba Mwenyezi Mungu ayafanye makubwa malipo ya familia yake na awajaalie kuwa mionganini mwa wenye subira wanaotaka malipo yake.

[إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ]

“Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea.” [Al-Baqara:156]

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

**katika Wilayah Jordan**